OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZAMITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

Shule ya Sekondari Kalemela,

S. L. P 89

BUSEGA

13/12/2020

Mwanafunzi ……..

Shule ya Msingi……

BUSEGA

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KALEMELA WILAYA YA BUSEGA

MKOA WA SIMIYU MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka 2021. Shule ya sekondari kalemela ni yakutwa yenye wanafunzi mchanganyiko (wavulana na wasichana). Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** na mwisho wakuripoti ni tarehe **18/01/2021** ndani ya siku saba.**Usipo Ripoti Shuleni Ndani ya Muda Huo,Nafasi yako itachukuliwa na Waanafunzi wariokosa Nafasi.**

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 Sareyashule

i. Wavulana:-Suruali **DAMU YA MZEE**, mbili zenye malinda mawili kila upande, mkunjo wa chini “turn up” mzingokwachiniinchi 17.

ii. Wasichana:-Sketi ya **DAMU YA MZEE**, mbili zenye marinda 14 tu, zinazofika kwenye Vifundo vya Miguu..

iii. Mashati meupe mawili mikono mifupi.

iv. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye Kamba na visigino vifupi.

v. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili zisizo na mapambo.

vi. T- shirt ya Damu ya Mzee kwa ajili ya michezo na sweta la damu ya mzee kwa ajili ya baridi.

vii. **KWA WANAOVAA HIJAB**.Mashono ya nguo yazingatie maadili ya dini husika, suruali hairuhusiwi.

2.2 Vifaa vya kujifunzia:-Daftari kubwa 12, kalamu,Rim moja,rula na mkebe wa hesabu (mathematical set). **LAZIMA** kuwa na mfuko au begi la kutunzia vifaa hivyo.

2.3 Mahitaji mengine:-

- Ndoo ya lita 10.kwa Wavulana na Wasichana
- Wasichana Njoo na Fagio laini ya Ndani yenye mpini mrefu(Bloom) na Fagio ya Nje yenye mpini mrefu (ainayachelewa)
- Wavulana Njoo na Jembe (jipya) na mpini wake.

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sharia Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya RAIS – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi nauendeshaji elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ya fuatayo ambayo ya tafafanuliwa kwa maandishi na utapewa na kala yake mara baada ya kuripoti.

Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote,na kwa wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima ukizingatia ya fuatayo:-

a) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulinga na ratiba ya shule nilazima.
b) Kushiriki kwa makini kujifunza kwa bidii shuleni na nyumbani.
c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
h) Kutunza maliza umma.(Mf. viti,meza,ndoo,fagio miti n.k ni Muhimu)

3.1 MAKOSA YA FUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi
b) Uasherati na Ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule
g) Kudharau bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito / kupatamimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoamimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kumiliki / kuwa na simu ya mikononi

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa wilaya wa hospitali ya serikali. Form hiii takabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni **(KIAMBATANISHO B).**
b) Form ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai na mzazi/mlezi kukirikukubaliana na sharia, kanuni na maelezo mengine ya takayotolewa na shule **(KIAMBATANISHO A)**

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA KARIBU SANA KATIKA SHULE HII:

……

S. M. LAMECK

MKUU WA SHULE

KIAMBATANISHO 'A'

FOMU YA MKATABA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KALEMELA

ANUANI YA MZAZI/MLEZI……

……

……

Tarehe……

MKUU WA SHULE,

Shule ya Sekondari Kalemela,

S .L . P 89,

Busega.

SEHEMU 'A' IJAZWE NA MWANAFUNZI.

Mimi…….ambaye ni mvulana/msichana niliye kuwa na soma Shule ya Msingi……Wilaya ya **Busega,** Mkoa **Simiyu**, Nakubali kujiunga na Shule ya **Sekondari Kalemela iliopo** Wilaya ya **Busega** mkoa wa **Simiyu** leo tarehe ……Nitazingatia na **kutii Sheria** za Shule hii, nitakuwa **mwaminifu**, **mwenye bidii** na **juhudi** katika **masomo**,**kazi** za **nje** na **michezo.**

JINA LANGU……..SAHIHI……

TAREHE…….

SEHEMU 'B' IJAZWE NA MZAZI/MLEZI

Mimi…….Mzazi/Mleziwa……

Ninayeishi kitongoji cha ……Kijiji cha ……Wilaya ya **Busega** Mkoa wa **Simiyu**, Nakubali motto wangu kujiunga na kusoma katika Shule ya **Sekondari Kalemela** kuanzia Tarehe……..hadi atakapo hitimu kidato cha Nne. Mtoto wangu nitampatia **mahitaji yote** yanayo takiwa Shuleni. Nitahakikisha n**inafuatilia** kwa ukaribu sana **Mahudhurio, Mwenendo** na **Maendeleo yake Shuleni**. Hivyo sitasita kumwonya na kuchukua hatua za kisheria pale anapo bainika kutenda kinyume na Sheria, Kanuni na Taratibu za Shule.

JINA LANGU……..SAHIHI……

TAREHE…….

KIAMBATANISHO 'B'

APPLICATION FORM FOR MADICAL EXAMINATION

KALEMELA SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 89 BUSEGA

To be completed by medical officer in respect of all for one entrant.

Full name……

Age……years. Sex…….

Blood court(red and white)……..

Stool examination

……

Urine analysis ……..Gestation for girls……

TB Test……

Ear……..

Chest…..

Abdomen……

ADDITION INFORMATION:(eg.Physical defects/impairment infections or chronic disease require special
treatment)……
……
……

I certify that the above named student **is fit/unfit** to pursue the studies as stated above.

Signature……

Destination…….

Station …….

Date …….

N.B: Medical officer.

At a time of examination,please treat the individuals for any ailment you noted.